# Kuelewa IEP

## IEP ni Nini?

IEP ni Programu ya Elimu kwa Ajili ya Mtoto wako inayoundwa, kuhakikiwa, na kudurusiwa  katika mkutano.

Aidha IEP:

- Huongoza elimu ya mtoto wako au mwanafunzi mtu-mzima.
- Hutoa msingi kusaidia timu ya IEP kuamua kiwango cha kielimu anachowekwa mtoto wako.
- Lazima iandikwe ndani ya kipindi cha siku 30 za kalenda wakati  wakati mtoto wako amesemekana kwamba anahitaji huduma ya elimu  maalumu.
- Lazima ianze kufuatiliwa mwanzoni mwa kila mwaka wa masomo.
- Si mkataba kwa hivyo taasisi au walimu hawawezi kuwajibika kama mtoto hajafikia malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, walimu na watoa huduma za kitaaluma wanawajibika kutoa huduma jinsi ilivyoandikwa katika IEP.
- Lazima iandikwe katika mkutano ambao unahusisha wazazi. Baadhi ya wanachama wa timu watakuwa wameshiriki katika mchakato wa kutathmini na kuanisha.
- Lazima iandikwe kabla mtoto wako hajawekwa anakofaa na kuanzishwa kwa huduma.
- Inaudwa, inahakikiwa, na kudurusiwa kwa mujibu wa IDEA na Elimu Maalumu ya Jimbo la Utah Kanun.

## Je, Lengo la IEP ni Gani?



1. Inatumika kama chombo mawasiliano kati ya wanafunzi na wafanyikazi wa shuke, na kuwawezesha kama washiriki sawa kuamua pamoja; kwanza, ni nini mwanafunzi anahitaji; pili, ni malengo gani mwanafunzi atajitahidi kufikia, na tatu, ni huduma gani mwanafunzi atapewa zimsaidie kufikia malengo hayo.
2. Inatoa fursa ya kusuluhisha matatizo yoyote baina ya wazazi na wafanyikazi wa shule kuhusu mahitaji ya elimu maalumu ya mtoto mwenye ulemavu; kwanza, kupitia mkutano wa IEP, na pili, kama inabidi, kupitia kinga za kitaratibu ambazo zipo kwa ajili ya wazazi na shule.
3. Kimaandishi, hutoa hakikisho la kupata nyenzo muhimu kuwezesha mwanafunzi ulemavu kupokea elimu maalumu na huduma husika.

4. Ni kifaa cha usimamizi kusaidia kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye ulemavu anapewa elimu maalumu na huduma husika zinaafiki mahitaji ya masomo maalumu.
5. Ni hati ya kuafikia na kufuatilia ambayo inaweza kutumiwa na wafanyikazi kutoka kila kiwango cha serikali kuthibitisha kwamba mwanafunzi mwenye ulemavu anapokea elimu faavu ya umma (FAPE) iliyokubaliwa na wazazi na wanafunzi watu-wazima na shule.

## Je, IEP Inafaa Kuboreshwa na Kuhakikiwa Mara Ngapi?



Sheria uhitaji angalau mkutano mmoja wa timu kila mwaka unaozalisha IEP iliyoandikwa. Katika mkutano wa IEP, wazazo ma wafanyikazi

wa shule hutoa uamuzi wa pamoja kuhusu programu ya masomo ya mtoto mwenye ulemavu kwa msingi wa mahitaji ya mtoto ilivyobainishwa na tathmini. Hati ya IEP ni rekodi ya maandishi juu ya maamuzi yaliyoafikiwa katika mkutano.

## Ilani ya Mkutano

Mzazi au mwanafunzi mtu-mzima lazima apokee ilani ya mkutano inayoonyesha lengo, wakati na mahali pa mkutano na wale wataohudhuria. Ni lazima pia iwafahamishe kuhusu haki yao ya kuandamana na watu wengine wenye ufahamu au ujuzi maalumu.

Ilani ya mkutano inayohitajika kupewa wazazi au wanafunzi watu-wazima (miaka 18+) lazima:

- Iwe na lengo, wakati na mahali pa mkutano na ni kina nani watakaohudhuria.
- Iwafahamishe kuhusu ruhusa ya kushiriki ya watu wengine wenye ufahamu na ujuzi maalumu kuhusu wanafunzi walioko kwenye timu ya IPE.
- Kwa wanafunzi wanaoingia chekechea, wafahamishe wazazi kwamba kwa ombi lao, mratibu wa huduma ya Kitengo cha (Part C service) au mwakilishi wa mfumo wa Part C anaweza kushiriki katika mkutano wa mwanzo wa IEP kwa mwanafunzi ambaye awali alihudumiwa chini ya Part C (Usaidizi wa Mapema, miaka 0-3).

## Ilani ya mkutano kwa IPE ya Mpito wa:

Ilani ya IEP ya mkutano wa mwanzo wakati mwanafunzi ana miaka 14 au zaidi, au chini kama itapatikana kuwa mwafaka na timu ya IEP, lazima pia

- Ionyeshe kwamba lengo la mkutano litakuwa kufikiria malengo ya baadaye ya sekondari na huduma za mpito za mwanafunzi.
- Ionyeshe kwamba taasisi itachochea mwanafunzi.
- Ionyeshe kwamba mwakilishi wa taasisi nyingine amealikwa kwa ruhusa ya wazazi au mwanafunzi mtu-mzima.

## Je, Ni Nani Wanachama Wa Timu ya IEP?

IDEA ina upekee kuhusu wanachama wa timu ya IEP wanaohitajika, na nani anafaa kuhudhuria katika kipindi chote cha mkutano. Uanachama wa timu ya IEP utajumuisha:

- Mzazi mmoja au wote au mlezi au mzazi wa kupanga na mwanafunzi mtu-mzima wakati wa kupanga mpito(*kuanzia mwaka wanapoingia miaka 14) au wanafunzi wachanga, ufaavyo.
- Mwalimu wa elimu maalumu asiyepungua mmoja wa mwanafunzi, au ifaavyo, mhudumu asiyepungua mmoja wa elimu maalumu ya mwanafunzi.
- Angalau mwalimu mmoja wa elimu ya kawaida wa elimu ya mtoto, kama mtoto anashiriki katika mtaala wa jumla
- Mwakilishi wa Taasisi ya Elimu ya Eneo (LEA) ambaye kawaida ni msimamizi wa shule au mwakilishi. Mtu huyu amehitimu kutoa huduma au kusimamia utoaji wa elimu maalum na ana ufahamu kuhusu mtaala wa elimu kwa ujumla. Mwakilishi wa LEA pia ana ufahamu kuhusu uwepo wa rasilimali za LEA na ana mamlaka ya kuweka rasilimali zinazohitajika, ikiwemo fedha, za kutoa huduma za elimu kwa mtoto wako.
- Mtu ambaye anaweza kufasiri athari za ufundishaji wa matokeo ya tathmini. Wakati mwingine huyu ni mtu ambaye tayari ni mwanachama wa timu, kama vile mwalimu.
- Kwa hiari ya mzazi au mwanafunzi mtu-mzima au shule, watu wengine wenye ufahamu au au ujuzi maalumu kuhusu mwanafunzi, pamoja na mtoa huduma zinazohusiana ifaavyo (Mtu ambaye atatoa mialiko ndiye anaamua ni nani mwenye ujuzi.



## Mahudhurio ya Timu ya IEP

Mwanachama wa timu ya IEP hahitajiki kuhudhuria mkutano wote wa IEP, au sehemu yake, kama mzazi wa mwanafunzi au mwanafunzi mtu-mzima mwenye ulemavu na LEA wamekubaliana, kimaandishi, kwamba kuhudhuria kwa mwanachama si muhimu kwa sababu eneo la mtaala au huduma ya huyo mwanachama haibadilishwi au kujadiliwa katika mkutano.

Mwanachama wa timu ya IEP anaweza kuruhusiwa kutohudhuria mkutano wote wa IEP, au sehemu yake, wakati mkutano unahusisha marekebisho ya mjadala wa eneo la mtaala wa mwanachama au huduma husika tu kama:

- Mzazi au mwanafunzi mtu-mzima na LEA wote wamekubaliana kutohudhuria huko kimaandishi, na;
- Na mwanachama kuwasilisha, kimaandishi kwa mzazi na timu ya IEP, mchango kwa uundaji wa IEP kabla ya mkutano.
- Uamuzi juu ya hitaji la mwanachama wa IEP kuhudhuria lazima ufanyike wakati wa mkutano mmoja na mwingine.



## Kushiriki na Kuhudhuria kwa Mzazi

LEA lazima ichukue hatua kuhakikisha kwamba mmoja au wazazi wote wa mwanafunzi mwenye ulemavu au mwanafunzi mtu-mzima wapo katika kila mkutano wa IEP au wamepewa fursa ya kushiriki, ikiwa ni pamoja na:

- Kuwaarifu wazazi kuhusu mkutano mapema iwezekanavyo kuhakikisha wamepata fursa ya kuhudhuria.
- Kuratibu mkutano katika mahali na wakati uliokubalika kwa pamoja.
- Kama hakuna mzazi anaweza kuhudhuria, lazima LEA itumie mbinu nyingine

kuhakikisha mzazi amehudhuria, pamoja na njia mbadala za kushiriki mkutano kama vile video au simu za wengi. Mzazi wa mwanafunzi mwenye ulemavu na LEA wanaweza kukubaliana kutumia njia mbadala ya kushiriki mkutano, kama vile video na simu za wengi.

Mkutano unaweza kufanyika bila mzazi au mwanafunzi mtu-mzima kuhudhuria kama LEA atashidwa kuwashawishi wazazi kuhudhuria. Katika hali hii, LEA anafaa kuweka rekodi ya juhudi zake za kujaribu kupanga kwa pamoja wakati na mahali.




## Kujiandaa kwa ajili ya mkutano wa IEP Mawaidha kwa wazazi

Kujiandaa kwa ajili ya mkutano wa IEP kunaweza kusaidia wazazi kushiriki maelezo vizuri na timu na kushiriki kwa njia ifaayo kakamavu katika mchakato. Kushiriki kwa mzazi ni kitu muhimu katika kuamua huduma inayofaa zaidi kwa mtoto.

Yafuatayo ni mapendekezo ya jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya mkutano:

- Kusanya habari za kushiriki: za kimatibabu, kisaikolojia, tathmini nyinginezo, vidokezo kuhusu ni kitu gani hufanya kazi vizuri kwa mtoto wako nyumbani, mbinu za awali zilizomfaa akiwa shuleni, hali ya sasa ya familia au matatizo.
- Hakiki rekodi ya mtoto wako shuleni na IEP ya sasa kama unayo moja.
- Orodhesha kile unachokiona kama uwezo na mahitaji ya mtoto wako.
- Andika mambo ya kipaumbele na malengo ya muda mrefu ya mtoto wako.
- Orodhesha huduma unazoamini mtoto wako anahitaji ili kufikia malengo umeyatambua.
- Andika chini maswali yako.
- Hakikisha mkutano wa IEP utakuwa mrefu vya kutosha ili kujadili yote unayohitaji yajadiliwe. Kuwa mwenye kuelewa, lakini kama muda utaishia timu, unaweza kuomba mkutano mwingine uratibiwe ili mchakato ukamilike.

## Wasiliana na timu yako kabla ya mkutano:



- Wapashe kuhusu ni nani umealika kwenye mkutano.
- Ombao uone mswada wa malengo ya IEP.
- Omba takwimu za tathmini uhakiki.
- Ikihitajika, omba upewe tafsiri ya lugha na upokee nyenzo katika lugha yako ya mwanzo.
- Usaidizi wowote unaohitajika kushiriki katika mkutano, kama vile wakalimani au nyenzo katika muundo unaoweza kuzifikia.

## Ujuzi wa Mawasiliano Unaofaa Kwa Wazazi



Wewe ndiye mtetezi mkuu wa mtoto wako. Una ufahamu maalumu wa mtoto wako. Usidhani kwamba shule ina kila maelezo yanayofaa. Kushiriki maelezo kunakusaidia wewe na timu ya shule yako kuelewa mtoto wako na kubuni masuluhisho yanayowezekana.Zungumza na mtoto wako upate kuelewa anayoyapitia akiwa shuleni ni gani anavyohisi.

Kuna mambo mengine mbali ya maneno ambayo yanaathiri jinsi wengine huelewa mawasiliano yetu. Haya ni pamoja na ishara za mwili, hali ya sauti, ukumbwa wa sauti, kuangaliana kwa macho, ishara za uso, ishara zamikono na upashaji ujumbe. Zingatia haya ukiwa na wengine.

## Kuwa msikilizaji mjuzi

Msikilizaji mjuzi ni mtu ambaye..

- yuko tayari kufanya juhudi kusikiliza.
- anasikiliza ujumbe wote kabla ya kuanza kujibu.
- anasikiliza maudhui, na sio jinsi ujumbe unavyofikishwa.
- anapuuzilia mbali usumbufu na kuazingatia kiini.
- anasikiliza mambo makuu na muhimu.
- anasikiliza kuelew mtazamo wa mwingie, badala ya kujishughulisha kufikiria atakavyomjibu.

## Kubaliana na Hisia

Kukubaliana na hisia anazoelezea mwingine zinamfanya mtu kufahamu kwamba unamsikiliza na kwamba unahisi hisia zao. Hili usaidia kutuliza hisia nzito ambazo huzuia mawasiliano.

## Tumia Kauli za “Mimi ni”

Kauli za "Mimi ni" huangazia mashaka, jinsi unavyohisi, na unachokifikiria. Zinawafanya wengine wasijifikire kana kwamba wanahukumiwa, wanashtumiwa au kutishwa. Zinapotumiwa, wengine huwa wana hiari ya kukusikiliza, wanasikiliza mashaka yako na kushirikiana kwa pamoja kupata masuluhisho ya mtoto wako.

## Uliza Maswali

Kupata ufafanuzi...

- kunakusaidia kuelewa kinachozungumzwa.
- kunakusaidia kufapa maelezo zaidi.
- kunakusaidia kupima matarajio, mashaka au mitazamo ya mtu mwingine.
- kunaeleza kinachoendelea kufanywa ili kusaidia.
- kunaweza kukusaidia kuelekeza mjadala katika eneo unahisi linahitaji kuzingatiwa.
- kunakusaidia kupata maelezo kabla ya kutoa maoni yako au kufanya makisio.
- kunaweza kutumiwa kupunguza kasi ya mazungumzo na kukupa muda kumeng'enya maelezo.

## Kile Sahihi Yako Inamaanisha:

- washiriki wote wanafaa kusaini IEP.
- Sahihi zote kwenye IEP huonyesha kushirki na mahudhurio.
- Wazazi wanaweza kuandika kwenye IEP kwamba “hawakubaliani” au wana mashaka.

